TANGAZO LA SERIKALI NA. 76 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA MBAGALA YA MWAKA, 2023

| | |
|---|---|
| Jina | 1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mbagara ya Mwaka, 2023. |
| | |
| Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355 | 2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango miji. |
| | |
| Mpango katika eneo la kwenye Jedwali | 3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Mafinga. |

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya ya mpaka ya upimaji namba HMU 49 yenye maira - nukta 752751.000MS, 9084253.791KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.61 hadi kwenye makutano ya mto Kinyapera kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBL 01 yenye majira - nukta 753357MS, 9084343KZ; baada ya hapo mpaka unafuata mto Kinyapera kwa umbali wa kilomita 1.93 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBL 02 yenye majira - nukta 752306MS, 9083535KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.42 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MBL 03 yenye majira - nukta 752477MS, 9083922KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.22 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMT 894 yenye majira - nukta 752688.879MS, 9083877.579KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.26 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMT 918 yenye majira - nukta 752751.000MS, 9084129.944KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba HMU49 hadi ulipoanzia''

Dodoma,
………., 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*